JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

MAELEKEZO KWA MAKARANI WAONGOZAJI WAPIGA KURA

UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2010

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI
POSTA HOUSE
MTAA WA OHIO
S.L.P. 10923,
DAR ES SALAAM

SIMU: +255 22 2114966
FAKSI: +255 22 2116740/2113382/2129852
Barua pepe: uchaguzitanzan@yahoo.com
TOVUTI; www.nec.go.tz

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

MAELEKEZO KWA MAKARANI WAONGOZAJI WAPIGA KURA

UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI, 2010

UJUMBE WA MWENYEKITI

Umeteuliwa kuwa Karani Mwongozaji Wapiga Kura na umepewa jukumu la kuwaongoza Wapiga Kura mahali pa Kupiga Kura zao Siku ya Uchaguzi.

Kwa muda wa miezi kadhaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi pamoja na Watendaji mbalimbali wa Uchaguzi wamekuwa wakifanya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao.

Mafanikio ya Uchaguzi yatatokana na Wewe kutekeleza jukumu lako kwa ufanisi ili kuwezesha Wapiga Kura wote kupata fursa ya kupiga kura zao bila kuhangaika.

Nakutakia kila la kheri na mafanikio katika kazi yako.

(Jaji Mstaafu Lewis M. Makame)
MWENYEKITI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

UTANGULIZI:

Uchaguzi Mkuu utahusisha Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Maelekezo haya yanahusu utekelezaji wa shughuli katika Vituo vya Kupigia Kura na yamezingatia Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985 (Sura ya 343), Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya mwaka 1979 (Sura ya 292) na Kanuni za Uchaguzi. Maelekezo haya yanawahusu Makarani Waongozaji Wapiga Kura.

Unapaswa uyasome Maelekezo haya muhimu na kuyaelewa ili uweze kutekeleza vizuri wajibu wako. Vile vile kama Watendaji wengine Kituoni ili kufanikisha zoezi hilo muhimu, unatakiwa kutumia lugha nzuri, hekima, busara na uvumilivu wakati unatoa huduma kwa Wapiga Kura Vituoni.

(Rajabu R. Kiravu)
MKURUGENZI WA UCHAGUZI

MAELEKEZO YA MAKARANI WAONGOZAJI WA WAPIGA KURA KATIKA VITUO VYA KUPIGIA KURA (DIRECTION CLERKS)

1.0 Utangulizi

Makarani Waongozaji wa Wapiga Kura (Direction Clerks) ni Watendaji wanaoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa ajili ya kuwaongoza Wapiga Kura kwa kuwaelekeza vituo ambavyo Wapiga Kura hao wamepangiwa. Watafanya hivyo kwa kufuata Orodha ya Wapiga Kura iliyotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Maelekezo haya yanakusudia kuelezea juu ya Uteuzi, Mafunzo, Majukumu na Wajibu wa Makarani Waongozaji wa Wapiga Kura kwenye Vituo vya Kupigia Kura.

2.0 Uteuzi Wa Makarani Waongozaji Wapiga Kura Katika Vituo

Uteuzi wa Makarani Waongozaji wa Wapiga Kura utafanywa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa kufuata maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Makarani Waongozaji Wapiga Kura wanapatikana baada ya Msimamizi wa Uchaguzi katika Halmashauri husika kutangaza nafasi za kazi hiyo zinazohitajika kujazwa. Baada ya zoezi la kutangaza nafasi hizo, hatua mbalimbali za kupokea maombi na kuchambua walio na sifa zitafanyika. Baada ya Orodha ya walio na sifa kukamilika watafanyiwa usaili na kasha Msimamizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi rasmi kwa wale wenye sifa.

3.0 Sifa Za Karani Mwongozaji Wapiga Kura

Karani Mwongozaji wa Wapiga Kura ni mtu yeyote aliyeteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi na ambaye anazo sifa zifuatazo;

(i) Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne na anayeweza kuyaelewa Maelekezo yanayotolewa na Msimamizi wa Uchaguzi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhusiana na majukumu yake Kituoni.

(ii) Awe raia wa Tanzania na ni vizuri awe mkazi wa eneo ambapo vituo/kituo hicho kipo.

(iii) Ikiwezekana awe mkazi wa Kata ambayo atafanyia kazi ya kuongoza Wapiga Kura.

(iv) Ikiwezekana awe Mpiga Kura wa Kituo anachofanyia kazi husika.

(v) Awe mwadilifu, mvumilivu, mpole, msikivu na anayeweza kufanya kazi kwa kujituma.

(vi) Asiwe shabiki wa Chama chochote kile cha Siasa.

(vii) Awe tayari kutoa msaada kwa Mpiga Kura yeyote atakayehitaji msaada wake bila upendeleo wala ubaguzi wa namna yoyote ile.

4.0 Mafunzo/Semina

Msimamizi wa Uchaguzi ataandaa semina au mafunzo kwa Makarani Waongozaji wa Wapiga Kura. Watapatiwa mafunzo ya siku moja na Msimamizi wa Uchaguzi ili waweze kuelewa vizuri taratibu zinazotakiwa na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Makarani Waongozaji wa Wapiga Kura watapaswa wafanye kazi zao kwa haki, kujiamini, kwa kuzingatia sheria, Kanuni na Maelekezo waliyopewa bila woga wala upendeleo.

5.0 Orodha Ya Wapiga Kura

Ili kuifahamu ipasavyo Orodha ya Wapiga Kura, Msimamizi wa Uchaguzi atampatia Karani Mwongozaji wa Wapiga Kura Maelekezo ya namna ambavyo Orodha hii imepangwa. Kwa kawaida Orodha hii huwa na mpangilio ufuatao:

(i) Kila kituo kinategemewa kuwa na jumla ya Wapiga Kura wasiozidi 450, ingawaje wakati mwingine wanaweza kupungua. Kwa mfano katika kituo cha kujiandikisha ambacho wameandikishwa Wapiga Kura 1,000, kituo hicho kitagawanywa katika vituo A, B na C. Kituo cha "A" kitakuwa na Wapiga Kura 333, Kituo cha "B" kitakuwa na Wapiga Kura 333 na Kituo cha "C" kitakuwa na Wapiga Kura 334.

(ii) Orodha ya majina itakuwa imepangwa kwa kufuata mtiririko wa kiherufi (alphabetical order), kwa

kuzingatia jina la kwanza la mpiga Kura kama alivyojiandikisha (kama vile Hadija Salum, atapatikana kwenye "H", Khadija Salum, atapatikana kwenye "K" na Adija Salum atapatikana kwenye "A").

Mgawanyo wa Wapiga Kura katika kituo cha kupigia kura hugawanywa na mfumo wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Sehemu ambayo kuna Vituo vya kuandikisha Wapiga Kura zaidi ya kimoja yaani A, B na C na vituo hivyo vimeandikisha Wapiga Kura wengi Vituo hivyo vitagawanywa katika utaratibu ufuatao; kwa mfano:

Kituo A kimeandikisha Wapiga Kura 800
Kituo B kimeandikisha Wapiga Kura 1,000
Kituo C kimeandikisha Wapiga Kura 1,500
Kituo A kitagawanywa mara mbili yaani AA, AB.
Kituo B kitagawanywa mara tatu yaani BA, BB, BC.
Kituo C kitagawanywa mara 4 – CA, CB, CC, CD.

Kila kituo kitakuwa na Majina ya Wapiga Kura majina yanayoanzia herufi A hadi Z.

Hivyo Mpiga atakapokuja muombe akuonyesha kadi yake kisha angalia yupo katika kituo gani cha kujiandikisha/kupigia kura na kama ni Kituo chako mwelekeze katika Kituo husika.

Angalizo: Kama shule ya msingi ina Vituo vitatu kama ilivyooneshwa katika mfano hapo juu majina yanayoanza na herufi H mfano yanaweza kuwa katika kituo A, au B au C.

6.0 Wajibu Na Majukumu Ya Makarani Waongozaji Wa Wapiga Kura

Majukumu ya Makarani Waongozaji wa Wapiga Kura ni kama ifuatavyo:

(i) Kuwapokea Wapiga Kura wanaokuja kituoni na kuwaelekeza mahali wanapopaswa kupiga Kura zao.

(ii) Kuhakiki kadi za Wapiga Kura wasiojua mahali wanapopaswa kupiga Kura kwa kulinganisha taarifa zilizomo kwenye kadi za Wapiga Kura na zile zilizomo kwenye Orodha ya Wapiga Kura.

(iii) Kutoa maelekezo kwa Wapiga Kura wanaokuja kituoni, mahali/vyumba wanapostahili kupigia Kura zao na kuhakikisha kuwa jina lililoko kwenye kadi ndilo lililoko kwenye Orodha ya Wapiga Kura.

(iv) Kuwasaidia Wapiga Kura ambao ni Walemavu, wakina mama Wajawazito, Wagonjwa, Wazee na Vikongwe ili waweze kupewa kipaumbele kupiga Kura zao kwa mujibu wa maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

(v) Ashirikiane na Watendaji wa Kituo katika kufanikisha shughuli za Upigaji Kura Kituoni.

(vi) Iwapo atashindwa kupata majina ya Wapiga Kura husika waliokuja Kituoni awaelekeze (wale walio na simu za mkononi) watumie mtandao wa simu ya mkononi kwa kutuma ujumbe mfupi SMS. Mpiga Kura atapaswa afuate Maelekezo yafuatayo:-

(a) Afungue Simu yake upande wa kuandika ujumbe mpya (SMS).

(b) Aandike 3, ikifuatiwa na Namba ya Mpiga Kura.

(c) Asisahau kuweka alama ya mkato (,) kati ya tarakimu 3 na namba ya kadi yake.

(d) Atume ujumbe huo kwenda Namba 0753 – 123179.

(e) Asubiri kupata jibu na asirudie kutuma ujumbe kabla ya kupata jibu kwa kuwa mtandao unachukua muda kutafuta taarifa hizo.

(vii) Atawajibika kwa Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura.

7.0 Hitimisho

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikifanya jitihada ya kuboresha utendaji wa shughuli za Uchaguzi ikiwemo upigaji

Kura. Uteuzi wa Makarani Waongozaji Wapiga Kura umefanywa kwa nia njema ya kuwasaidia Wapiga Kura, kutambua vituo walivyopangiwa na kushiriki kupiga kura zao. Hivyo ni wajibu wa Watendaji hawa kufuata taratibu zilizowekwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Msimamizi wa Uchaguzi.